

JINA _____ KIDATO _____
TAREHE _____ SAHIHI _____

**102/3
FASIHI YA KISWAHILI
KIDATO CHA NNE
MUHULA WA KWANZA 2016
SAA 2 1/2**

**Cheti Cha Kuhitimu Elimu Ya Secondari Nchini Kenya
FASIHI YA KISWAHILI PP 102/3
KIDATO CHA NNE MUHULA WA KWANZA 2016**

Maagizo:

- Jibu maswali manne pekee
- Swalii la kwanza ni la **lazima**
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani : Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na Ushairi.
- Usijibu maswali **mawili** kutoka katika **sehemu moja**

Mtahiniwa ahakikishe kwamba karatasi hii ina kurasa 3 zilizopigwa chapa

Sehemu A: Fasihi Simulizi

1. LAZIMA

- a) Eleza majukumu yoyote manne ya fomyula ya ufunguzi wa ngano (alama 4)
- b) Taja aina zozote nne za ngano na kwa kila moja toa sifa mbili. (alama 12)
- c) Misimu ina majukumu gani katika jamii? (alama 4)

Sehemu B: riwaya- Kidagaa Kimemwozea- Kwn Walibora

Jibu swali la 2 au la 3

2. Huku ukirejelea mhusika Amani, onyesha ukweli wa kauli kwamba wema hatimaye huushinda uovu. (alama 20)
3. "Siwezi kuishi hemani humu mwituni kama maskini sina sinani nikiulizwa siungami"
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Fafanua sifa na umuhimu wa msemaji (alama 10)
- c) Dondoo hili linarejelea maudhui gani? (alama 2)
- d) Taja na ueleze tamathali mbili zilizotumiwa katika dondoo hili (alama 4)

Sehemu C: Tamthilia- Mstahiki Meya; Timothy Arege

Jibu swali la 4 au la 5

4. "Ndiyo hivyo bwana. Elimu yetu hapa ni ya kawaida mno. Haina kubwa la kumfaa mtoto mwenye mzazi anayeona mbali."
- a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)
- b) Taja na ueleze sifa zozote nne za msemaji (alama 8)
- c) Taja na ueleze maudhui yoyote manne yaliyoendelezwa na mnenaji (alama 8)
5. Jadili suala la utetezi wa haki katika tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 20)

Sehemu D: Hadithi Fupi- Damu Nyeusi na Hadithi Nyengine

Jibu swali la 67 au la 7

6. "Mimi nilitaka mke, mwanamke mbichi, nimvumbike mwenyewe mpaka aive"
- a) Liweke dondoo hili katika muktadha wake sahihi (alama 4)
- b) Ni kwa nini msemaji alitaka amvumbike mwanamke mwenyewe? (alama 2)
- c) Je, azma yake ilitimia? Eleza (alama 2)
- d) Eleza migogoro iliyochipuka baina ya msemaji na mwanamke huyu. (alama 12)
7. Huku ukirejelea hadithi zifuatazo, thibitisha kuwa mwanamke hajajikomboa kikamilifu
- i) Samaki wa Nchi za Joto (alama 20)
- ii) Mke Wangu
- iii) Ndoa ya Samani
- iv) Tazamana na Mauti
- v) Mwana wa Darubini.

Sehemu E: Ushairi

8.

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenyen zani, kweli mja hapendeki,
Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni nafiki,
Ukweli haafiki, njama zake zi moyoni, usimwone ni rafiki,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Wengine watakuua, akiona una pesa, hata zikiwa kidogo,
Hizo kwao ni maua, hupupiwa zikatesa, wakizifuata nyago,
Hadi kwenye kwako ua, pasipo hata kupesa, wala kukupa kisogo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Pindi kinunua kitu, hafurahi Shaitani, bali tajawa chukizo,
Mtu kiwa mtukutu, tanuna mtimani, kwalo lako tekelezo,
Tamko lake 'subutu', kuondoa tumaini, na kukuulia wazi,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Aliye taraghani, taabu kuishi naye, kazi yake kujidai,
Takusema faraghani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui,
Hana faida nyumbani, ni mtu akuchumbiye, mradi usitumai,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Kwa hakika ni balaa, kumkirimu mchawi, aliyejaa uchoyo,
Bahati ina hadaa, kukupa alo sodawi, aibatili rohoyo,
Mipangoyo kwake jaa, na nia ya ustawi, huwiza kuvunja kaniyo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Ninacho changu kilio, ninalia sanasana, kinyesi nimetupiwa,
Ningetoa azimio, lakini uwezo sina, kwa mazito kuambiwa,
Ama nitimue mbio, fuadini ninanena, akilini nazuiwa,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Maswali:

- a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama 2)
- b) Fafanua umbo la shairi (alama 4)
- c) Andika ubeti wa tatu kwa nathari (alama 4)
- d) Taja mifano miwili ya tamathali zilizotumiwa (alama 4)
- e) Eleza maana ya msamati huu kama ulivyotumika katika shairi:
i) Zani-
ii) Faraghani- (alama 2)
- f) Onyesha kwa kutoa mifano jinsi idhini ya mshari ilivyotumika (alama 4)